# KUANGAMIZWA KWA WATU WA NABII SALEH A.S

<"xml encoding="UTF-8?>

BSMILAHI AR-RAHMANI AR-RAHIIMI

KUANGAMIZWA KWA WATU WA NABII SALEH A.S

Kaumu ya Nabii Saleh A.S. iliangamizwa kwa sababu ya kumuuwa ngamia wa Mwenyezi Mungu na ilhali kabla ya hapo Mtume wao aliwaonya kwa onyo kali la kushukiwa na adhabu ya haraka kabisa ikiwa watamuuwa yule ngamia jike. Ingawa walionywa kwa hilo onyo kali lakini .hata hivyo watu wabaya hawakumsikia wala kumjali Mtume wao

Siku ya Jumatano wakamfukuza yule ngamia wa Mwenyezi Mungu na alipopita karibu ya Masda`a akamrushia mshale, na alipofika karibu na kijana aliyeitwa Qaddaar bin Saalif akamuuwa ngamia kwa upanga kwa amri ya wenzake. Kisha wakamchinja wakagawana nyama yake wakaila. Lakini mtoto wa ngamia aliwahi kukimbilia jabalini, na inasemekana aliingia " ,jabalini akapotea humo. Kama ilivyobainika katika Suratil Qamar aya ya 29

فَنَادَوْا صَاحِبَهُمْ فَتَعَاطَى فَعَقَرَ

Maana yake, "Basi wakamwita rafiki yao (Qaddaar naye kashika upanga) akamchinja (yule ngamia wa Mwenyezi Mungu wakamla)." Na pia Mwenyezi Mungu S.W.T. kasema katika Surat ,Sh-shams aya ya 14

فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُمْ بِذَنْبِهِمْ فَسَوَّاهَا

Maana yake, "Lakini walimkadhibisha (Mtume wao) na wakamchinja ngamia (wa Mwenyezi Mungu), kwa hivyo Mola wao aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na akawafuta kabisa ".((duniani

Basi khabari zile zilipomfikia Nabii Saleh aliwaambiya: "Nakutahadharisheni kukushukieni ile adhabu ya Mwenyezi Mungu niliyokuahidini kutoka mbinguni." Kama alivyosema Mwenyezi " ,Mungu S.W.T. katika Surat Huud aya ya 65

فَعَقَرُوهَا فَقَالَ تَمَتَّعُوا فِي دَارِكُمْ ثَلاثَةَ أَيَّامٍ ذَلِكَ وَعْدٌ غَيْرُ مَكْذُوبٍ

Maana yake, "Wakamchinja. Basi (Nabii Saleh) akasema "Stareheni katika mji wenu ( huu,

muda wa) siku tatu. Hiyo ni ahadi isiyokuwa ya uwongo." Baada ya kumuuwa yule ngamia wa Mwenyezi Mungu S.W.T. ambayo siku ile ilikuwa ni siku ya Jumatano, wakati wa usiku wake wale watu tisa wakaazimia na wakapanga mipango yao ya kutaka kumuuwa Mtume wao wakasema: Ikiwa kama kasema kweli kuwa itatujia adhabu basi sisi tumwahi kabla hatujawahiwa. Na ikiwa kama ni muongo tutakuwa tumemuuwa yeye na ngamia wake. Hivyo wakamwendea Nabii Saleh wakiifuata ile njia anayopitia wakati anapokwenda zake kusali Msikitini majira ya usiku, mara tu walipomkaribia, Mwenyezi Mungu S.W.T. akawarushia mawe wakafa wote kwa pamoja na vile vitimbi vyao vikenda patupu. Kama alivyosema Mwenyezi " ,Mungu S.W.T. katika Suratin Naml kuanzia aya ya 49 hadi 51

قَالُوا تَقَاسَمُوا بِاللَّهِ لَنُبَيِّتَنَّهُ وَأَهْلَهُ ثُمَّ لَنَقُولَنَّ لِوَلِيِّهِ مَا شَهِدْنَا مَهْلِكَ أَهْلِهِ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ * وَمَكَرُوا مَكْرًا وَمَكَرْنَا مَكْرًا وَهُمْ لا يَشْعُرُونَ * فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ مَكْرِهِمْ أَنَّا دَمَّرْنَاهُمْ وَقَوْمَهُمْ أَجْمَعِينَ

Maana yake, ""(Wale watu tisa) wakasema: "Apishaneni kwa Mwenyezi Mungu (ya kwamba) tutamshambulia usiku yeye (Saleh) na ahli zake, kisha tutamwambia mrithi wake: "Sisi hatukuona maangamizo (yake wala) ya watu wake na sisi bila shaka tunasema kweli. Basi wakapanga mipango yao, na Sisi tukapanga mipango yetu (tukapangua vitimbi vyao) na wao hawatambui. Basi angalia ulivyokuwa mwisho wa vitimbi vyao, tuliwaangamiza pamoja na watu ".wao wote

Ilipofika siku ya kwanza asubuhi ambayo ndio ilikuwa ni siku ya Alkhamisi, na ndio siku ambayo waliahidiwa na Nabii Saleh kushukiwa na ile adhabu, mara nyuso zao zikabadilika rangi ya manjano, na siku ya pili ambayo ilikuwa ni siku ya Ijumaa nyuso zao zikawa na rangi nyekundu. Na siku ya tatu ambayo ilikuwa ni siku ya Jumammosi nyuso zao zikawa na rangi .nyeusi, hata ikapita mchana wakafikiri kwamba wameokoka na ile adhabu

Lakini wapi! Ilipowapambazukia asubuhi ya siku ya nne ambayo ilikuwa ni siku ya Jumapili wakakaa wakiingojea ile adhabu ambayo hawakuijua ni adhabu gani, wala hawakujua itatokea mahali gani na wala hawakujua nini la kufanya. Ghafla tu lilipochomoza jua ikawaijia ile adhabu ya Mwenyezi Mungu S.W.T. kwa ukelele mmoja tu uliotoka mbinguni uliopigwa na Malaika Jibril A.S. ukawanyakuwa roho zao kisha ukafuatia mtetemeko mkali wa kutoka ardhini uliowatetemesha kwa nguvu kabisa mpaka wakafa wote katika nyumba zao wala hakuokoka ,hata mmoja wao. Kama alivyosema Mwenyezi Mungu S.W.T. katika Surat A`araaf aya ya 78

فَأَخَذَتْهُمْ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَاثِمِينَ

Maana yake, "Basi tetemeko la ardhi likawanyakuwa (roho zao), na kulipokucha wakawa

majumbani mwao kifudifudi wamekwishakufa."

,Na pia kama alivyosema Mola Mtukufu katika Suratil Qamar aya ya 31

إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ صَيْحَةً وَاحِدَةً فَكَانُوا كَهَشِيمِ الْمُحْتَظِرِ

Maana yake, "Kwa yakini tuliwapelekea ukelele mmoja tu, wakawa kama mabuwa ya kujenga uwa." Lakini Mwenyezi Mungu S.W.T. akamuokoa Mtume Wake pamoja na wale watu ,waliouamini ujumbe wake kama ilivyodhihirika katika Suratin Naml aya ya 53

وَأَنجَيْنَا الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ

".(Maana yake, "Na tukawaokoa wale walioamini na waliokuwa wakimcha (Mungu

MWISHO